

Please check the examination details below before entering your candidate information

Candidate surname

Other names

Centre Number

Candidate Number

--	--	--	--	--

--	--	--	--

Pearson Edexcel International GCSE (9–1)

Time 2 hours 15 minutes

Paper
reference

4SW1/01

Swahili

PAPER 1: Reading, Writing and Translation

You do not need any other materials.

Total Marks

Instructions

- Use **black** ink or ball-point pen.
- **Fill in the boxes** at the top of this page with your name, centre number and candidate number.
- There are **three** sections you must answer:
 - Section A Questions 1–4
 - Section B Question 5 and **either** Question 6(a) **or** 6(b) **or** 6(c)
 - Section C Question 7.
- Answer the questions in the spaces provided
 - *there may be more space than you need.*
- You must **not** use a dictionary.

Information

- The total mark for this paper is 80.
- The marks for **each** question are shown in brackets
 - *use this as a guide as to how much time to spend on each question.*

Advice

- Read each question carefully before you start to answer it.
- Check your answers if you have time at the end.

Turn over ►

P72389A

©2022 Pearson Education Ltd.

Q:1/1/1/



Pearson

SECTION A: READING

Answer ALL questions.

Write your answers in the spaces provided.

Multiple-choice questions must be answered with a cross ☒. If you change your mind about an answer, put a line through the box ☒ and then mark your new answer with a cross ☒. Open-response questions do not have to be written in full sentences and you may respond using single words or phrases.

- 1 Malizia sentensi zifuatazo kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Weka alama sahihi kwenye kila kisanduku.

Makumbusho ya Taifa

Jengo la makumbusho ya taifa ni kubwa na lina ghorofa tano. Ndani kumejaa michoro na vinyago vya sanaa kutoka kipindi cha kabla ya ukoloni hadi miaka ya sasa. Vitu vyote hivi vimetengenezwa kwa mawe, mbao au chuma; hakuna kitu kilichotengenezwa kwa dhahabu. Katika makumbusho, watu wazima na hata vijana wanaweza kugusa vitu vyote ambavyo vinaonyeshwa kwenye rafu au kwenye meza. Watoto hawawezi kugusa vitu isipokuwa kama kuna usimamizi wa watu wazima. Kuna ofisi ya mapokezi kwenye kila ghorofa ambapo maswali hujibiwa. Kuna ziara binafsi ambapo waongozaji huongoza watu ingawa malipo huhitajika kwa ziara hizi. Kwa kawaida hakuna malipo yoyote kwa watoto wenye umri ulio chini ya miaka sita.

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



A pesa

B dhahabu

C makumbusho

D vijana

E rafu

F mchoro

G huruhusiwa

H mbao

I swali

J hujibu

K ghorofa

L zilizopo

M bure

Example	Jengo la makumbuso lina ... tano	K
1 (a)	Kuna vinyago vya nyakati...	
1 (b)	Bidhaa inayokwepwa...	
1 (c)	Watoto ... kugusa vitu	
1 (d)	Wasaidizi wa mapokezi ... maswali	
1 (e)	Unahitaji ... kwa ziara binafsi.	
1 (f)	Kiingilio kwa watoto wadogo ni...	

(Total for Question 1 = 6 marks)



2 Weka alama katika visanduku **10** vilivyo sahihi. Sentensi nyingine au watu wengine wanaweza kuwa na alama zaidi ya moja au bila alama yoyote.

Maisha ya kila siku

Asha



Mimi ninatoka kwenye familia yenye watoto watano. Mimi na pacha mwenzangu tunapenda kufanya kila kitu pamoja. Zamani tulipenda kupanda farasi lakini mama alihisi kwamba ni hatari. Kila wikendi sisi huenda milimani na baisikeli ambapo tuna kibanda cha kupumzikia.

Sabrina



Wazazi wangu hawaishi pamoja na mama yangu si mpole. Pia si rahisi kuzungumza naye kwani amezoea kugombeza. Ningependa kuenda naye kufanya zoezi la kutembea lakini sidhani kama atakubali kwani anapenda kukaa peke yake. Kwa hivyo mimi hutazama runinga chumbani kwangu kutwa kucha. Siku zingine husoma riwaya.

Hirsi



Dada yangu anapenda sana kufanya mazoezi lakini mimi ninapendelea kutazama michuano ya mpira wa miguu kwenye runinga. Mara nyingi yeye hunifundisha masomo ambayo sijaelewa darasani. Shule inapofungwa sisi na wazazi wetu huenda kupumzika kijijini ambapo tuna shamba kubwa lenye ulinzi mkali.

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



		Asha	Sabrina	Hirsi
Mfano	Dada anapenda mazoezi	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
A	Husoma kama starehe	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
B	Usalama ni muhimu	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
C	Hafanyi shughuli peke yake	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
D	Mzazi anapenda nidhamu	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
E	Familia ina nyumba za kuenda likizo	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
F	Haendi popote wakati wa likizo	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
G	Ana ndugu anayempa msaada	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>

(Total for Question 2 = 10 marks)



- 3 Soma makala kuhusu Tamasha la Mavazi. Malizia taarifa kwa kutumia namba au maneno kwa **Kiswahili**.

Tamasha la Mavazi

Wikendi iliyopita kulikuwa na Tamasha la Mavazi ambapo tulikutana na wabunifu wa mavazi na wanamitindo wengi.

Kuliandaliwa mengi ikiwa ni pamoja na vyakula kama mihogo ya kuchoma na mishikaki, pia vikundi vya ngoma za kijadi vilionyesha ustadi wao. Ngoma niliyoipenda mimi ni ile ya Waluguru ambayo kihistoria ilichezwa ili kuita mvua. Watu walitania kwamba kama mvua ingalinyesha basi tungalipata tabu kwani tamasha lilifanyika katika uwanja mkubwa wa kandanda.

Kawaida tamasha hili hufanyika jijini Dar es Salaam ambapo kuna msongamano wa watu. Mwaka huu limefanyika mjini Morogoro ambapo kuna milima. Kwa hivyo vijana kama mimi ambao hatuishi Dar es Salaam, tumepata nafasi ya kujifunza mengi. Nimegundua kuwa utafiti na uuzaji wa bidhaa ni nyanja zinazokua. Pia nimeweza kuona kwamba tasnia ya mavazi na mitindo imekua sana nchini. Sasa ninajiuliza tamasha la mwaka ujao litakuwa wapi?

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

Mfano: Tukio: Maonyesho ya Mavazi

- (a) Wahusika ni pamoja na: na (2)
- (b) Shughuli kwa waliohudhuria: na (2)
- (c) Sababu ya kihistoria ya kucheza ngoma: (1)
- (d) ingeleta changamoto kwenye sherehe (1)
- (e) Sifa ya Dar es Salaam ni: (1)
- (f) Mandhari ya Morogoro (1)
- (g) Kuna nafasi za ajira katika: na (2)
- (h) Kuna maendeleo kwenye husika (1)
- (i) Mwandishi ana hamu ya kujua: (1)

(Total for Question 3 = 12 marks)



- 4 Soma habari ifuatayo kutoka kitabu kiitwacho **Damu Nyeusi**, kilichohaririwa na K Walibora na Said Mohamed.

Gilasi ya mwisho

Msoi alikuwa na wasiwasi lakini hakujua sababu. Rafiki yake, Semkwa, alikuwa na furaha na alitaka kuenda kwenye sherehe. Msoi alimweleza Semkwa kwamba yeye hakutaka kutoka kwa sababu alihisi balaa kubwa ingetokea.

Semkwa alimbembeleza sana rafiki yake watoke pamoja. Ilipofika saa mbili usiku, alienda kwa rafiki yake na kumkuta Msoi amelala juu ya sofa.

'Umejilaza kochini kama mgonjwa wa Malaria. Sasa ndiyo umegoma kutoka au?' alilalamika Semkwa.

'Sio hivyo...' alijibu Msoi.

'Sio kivipi? Hebu waachie wazee hizo imani za kishirikina. Sisi ni vijana na tunaendesha maisha yetu kisayansi. Hebu vaa tuende' alihimiza Semkwa.

Msoi aliinuka pale kochini kwa moyo mzito na shingo upande. Akaenda kukoga na kuvaa. Wakati walipokuwa wanatoka, Msoi alijikwaa kwenye kizingiti cha mlango na kutaka kuanguka, Semkwa akawahi kumshika mkono na kumcheka.

Walipoingia tu garini, mvua kali ilianza kunyesha. Halafu baada ya sekunde chache, radi kali ilipiga. Papo hapo Msoi alitazama nje ya gari na kuanza kufikicha mikono, alitamani kurudi nyumbani...

Jibu maswali kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Si lazima kuandika sentensi kamili.

- (a) Nini tofauti ya hisia za Msoi na Semkwa kuhusu kuenda kwenye sherehe?
Taja maelezo **mawili**.

(2)

- (b) Tunajuaje kwamba Semkwa ni mkaidi?
Taja maelezo **mawili**.

(2)



(c) Kwa Semkwa kuna tofauti gani za rika tofauti?
Taja maelezo **mawili**.

(2)

(d) Nini maana ya 'moyo mzito na shingo upande'?

(1)

(e) Kwa nini Semkwa alicheka baada ya Msoi kujikwaa?

(1)

(f) Tunajuaje kwamba Msoi ana wasiwasi?
Taja maelezo **mawili**.

(2)

(Total for Question 4 = 10 marks)

TOTAL FOR SECTION A = 38 MARKS



SECTION B: WRITING

Answer Question 5 and **either** Question 6(a) **or** 6(b) **or** 6(c).

Write your answers in the spaces provided.

5

Shule

Kumbukumbu

Kufika shuleni mapema

Muda wa masomo kuwa mrefu

Shughuli ufanyazo baada ya shule

Andika takriban maneno 70 kwa **Kiswahili** kuhusu shule. Ni lazima kutumia maneno yote yaliyotajwa hapo juu.

(12)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

Handwriting practice area with 25 horizontal dotted lines.

(Total for Question 5 = 12 marks)



P 7 2 3 8 9 A 0 1 1 1 6

6 Chagua **moja** kati ya maswali matatu yafuatayo na andika takriban maneno 130 kwa **Kiswahili**.

Chaguo 1

(a)



Andika hotuba kuhusu kuishi kwenye bwani la wanafunzi. Ni lazima uandike kuhusu:

- Umuhimu wa kuishi kwa kujitegemea
- Kumbukumbu ya kuishi maisha ya bwani
- Athari za baadaye za kuishi kwenye bwani

(20)

Chaguo 2

(b)

Mpendwa Hannah

Ninakuandikia barua pepe hii huku nikiwa pembezoni mwa barabara kwani basi letu limeharibika. Nilikuwa njiani kuenda Nairobi.

Vipi hali yako?

Rafikiyo,

Aaliyah

Jibu kwa kutumia barua pepe. Ni lazima uandike kuhusu:

- Hisia zako kuhusu Aaliyah
- Kumbukumbu yako ya tatizo ulipokuwa safirini
- Mipango yako kuhusu safari za baadaye

(20)



Chaguo 3

(c) Kwenye ukurasa wako wa blogu andika kuhusu mji unaoishi. Ni lazima uandike kuhusu:

- Vivutio vikuu
- Vitu upendavyo katika mji huo
- Mipango ya baadaye ya mji

(20)

Indicate which question you are answering by marking a cross ☒. If you change your mind, put a line through the box ☒ and then indicate your new question with a cross ☒.

Question 6(a)

Question 6(b)

Question 6(c)

Area with horizontal dotted lines for writing the answer.



P 7 2 3 8 9 A 0 1 3 1 6

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

(Total for Question 6 = 20 marks)

TOTAL FOR SECTION B = 32 MARKS



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

SECTION C: TRANSLATION INTO SWAHILI

Write your answer in the space provided.

7 Tafsiri aya ifuatayo kwa **Kiswahili**.

Electric Vehicles

Technology is developing rapidly. One of the latest development of technology that we can see in Africa is the possibility of driving electric vehicles. They are one of the best things to happen in the present day as they assist the global effort to reduce pollution.

South Africa has a number of electric cars already and there are about 180 charging stations. In addition to this, African countries such as Kenya and Rwanda have started encouraging their use by reducing vehicle taxes.

Area with horizontal dotted lines for writing the answer.

(Total for Question 7 = 10 marks)

TOTAL FOR SECTION C = 10 MARKS

TOTAL FOR PAPER = 80 MARKS



P 7 2 3 8 9 A 0 1 5 1 6



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

BLANK PAGE

Source information

Question 2

- © andresr/Getty Images
- © andresr/Getty Images
- © Getty Images

Question 6

- © FlamingoImages/Getty Images

